UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Kusomwa kwa Bajeti: Adhabu ya kila mwaka ya serikali dhidi ya raia wa kawaida.

**HABARI NA MAONI**
Wakoloni wa Magharibi Kufadhili Elimu ili Kuendeleza Utumwa wa Kifikra

**TOLEO JIPYA**
Masuali 3 kwa Majeshi ya Waislamu Kutoka kwa Vijana wa Kiislamu wa Magharibi

**JIBU LA SWALI**
Je, Yajuzu kwa Mwanamke Kafiri Kutawalishwa Ukadhi wa Shariah?

# #MWACHILIENI NAVEED BUTT



Msemaji rasmi wa Hizb ut-tahrir wilaya ya Pakistan

بسم الله الرحمن الرحيم

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 12/1442 | Ijumaa, 30 Shawwal 1442 H | 11/06/2021 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Kusomwa kwa Bajeti: Adhabu ya kila mwaka ya serikali dhidi ya raia wa kawaida

Alhamisi Tarehe 10, Juni 2021 waziri wa fedha Ukur Yattani alisoma bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2021 ya Shilingi trilioni 3.632. Bajeti hii ambao ndio kubwa zaidi kuwahi kusomwa katika historia ya Kenya ina nakisi ya shilingi trilioni 1.2. Kima cha shilingi trilioni 1.97 cha bajeti hii kinatarajiwa kukusanywa kupitia utozwaji ushuru huku kiwango cha shilingi trilioni 1.63 kikichukuliwa kutoka mikopo na ruzuku. Mamlaka ya mapato ya Kenya inatazamia kukusanya shilingi bilioni 835 huku kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ikitarajiwa shilingi bilioni 472.9 na ushuru wa uzalishaji katika bidhaa ukikisiwa kuwa kiwango cha bilioni 241.

Harakati ya Hizb ut-Tahrir Kenya ingependa kutaja yafuatayo;-

Bajeti hii inawasilishwa katika kipindi ambacho raia wa kawaida wamejawa na wasiwasi juu ya mkopo kutoka kwa shirika la Fedha duniani IMF wa jumla ya kitita cha shilingi bilioni 255 uliochukuliwa na Nairobi kwa lengo la kupunguza nakisi ya sasa ya fedha. Hatua hii imeilazimu serikali ya Kenya katika miaka ya hivi karibu itumie zaidi ya nusu ya ushuru kulipia mikopo yake. Ni wazi kwamba bajeti ya mwaka wa 2021/2022 kama zilivyo bajeti zozote zile ndani ya serikali za Kibepari humaanisha kuudhibu mamilioni ya wakenya ili kuingiza mikono yao zaidi mifukoni huku tayari wakikabiliana na mfumoko wa bei uliofanya bei za bidhaa msingi kama vile unga wa ngano na mafuta ya kupikia kupanda maradufu zaidi. Kwa uhakika haya ndio matunda ya mfumo muovu wa kirasilimali unaofanya mfumo wa fedha wa riba ndio msingi wa kupeleka uchumi wake hali inaopelekea mirundiko na mizigo ya madeni huku ukiongeza kiwango cha kulipia deni. Ni bayana kwamba Bajeti zinachorwa kwa misingi ya IMF na Benki ya dunia huletea taifa maafa zaidi ya kiuchumi bali kuifanya kuwa mateka ya kiuchumi.

Tofauti na Uislamu ambapo ukusanywaji wa ushuru hauzingatiwi sio wenye kuendelea bali ni kwa dharura tu, bajeti za kirasilimali zinazofanya mzigo wote wa matumizi yake kuegemea zaidi utozwaji mkubwa wa ushuru huku nakisi yake ikifidiwa na madeni na ruzuku. Na kwa muktadha huu ndio twasema kuwa taarifa za bajeti za kirasilimali hujumuisha vifungu vinavyoletea raia ugumu zaidi wa kiuchumi bali vikijumuisha matumizi ya kifahari na tarakimu kubwa ambapo huishia kuwapa wanasiasa uwezo wa kupora mabilioni ya pesa.

Dola ya Khilafah ambayo kwa Idhini ya MwenyeziMungu SWT kusimama kwake ni kwenye kukurubia siku hadi siku, haitopoteza wakati wa kujiweka michakato ya uhusiano mwema kusoma bajeti za kila mwaka hii ni kwa kuwa mapato na matumizi ya yake tayari yapo kwani yamekwisha elezwa na sheria za MwenyeziMungu. Khilafah haitotoza ushuru kwenye mishahara yao (PAYE) ama ushuru wa kimapato kwani ina vyanzo vya kupata mapato ya umma kama vile rasilimali kama vile madini ambapo zitaweza kutumiwa kuweza kukimu mahitaji ya raia pasina kuumiza watu katika ushuru. Kwa mapenzi ya MwenyeziMungu, kusimamishwa Khilafah ndio kutakapokomboa walimwengu kutokana na dhulma za kitawala na umasikini uliozagaa.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari, Hizb ut -Tahrir in Kenya**

 Email: info@uqab.or.ke

**Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وعد الله الذين آمنوا منكم وعملوا الصالحات ليستخلفنهم في الأرض كما استخلف
الذين من قبلهم وليمكنن لهم دينهم الذي ارتضى لهم وليبدلنهم من بعد خوفهم أمنا
يعبدونني لا يشركون بي شيئا ومن كفر بعد ذلك فأولئك هم الفاسقون﴾

KUMB: 38/1442 | Alhamisi, 29 Shawwal 1442 H | 10/06/2021 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Wito wa Kutaka Kumalizwa kwa Kupotezwa kwa Nguvu kwa Naveed Butt Nchini Pakistan

Ni miaka tisa sasa tangu Huduma za Ujasusi za Pakistan (ISI) kumteka nyara Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir katika Wilayah ya Pakistan, Mhandisi Naveed Butt, mnamo Mei 11, 2012. Kuhusiana na tukio hili, Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah ya Pakistan imetoa taarifa mbili kwa vyombo vya habari:

Ya kwanza mnamo 03/01/2021 kwa anwani: "**Agizo la Kumtoa Naveed Butt Lilitolewa Mnamo 4 Januari 2018, lakini Angali Hajaonekana wala Kuskika Tangu Kutoweka Kwake kwa Kulazimishwa mnamo 11 Mei 2012.**"

Ya pili mnamo 02/05/2021: "**Katika Kipindi cha Mwezi Uliobarikiwa wa Ramadhan, Wito wa Kuachiliwa Huru Naveed Butt, Mtetezi Halisi wa Khilafah, Aliyetekwa Nyara Tangu Mnamo 11 Mei 2012.**"

Naveed alikuwa mtu wa kisawasawa kutoka Lahore, mlezi wa familia, mhandisi wa umeme, Muislamu mwenye ikhlasi, mtu wa tabaka nadra miongoni mwa wanafikra wa kisiasa na kimkakati, na msemaji rasmi wa chama cha kale cha kisiasa Hizb ut Tahrir / Pakistan. Hii ni orodha fupi tu ya sifa zake, lakini hakuna hata moja ya haya lililokuwa umuhimu kwa ISI wakati Naveed aliposukumwa kuingia kwenye moja ya "**gari maarufu za Suzuki zenye sifa mbaya**", na kundi la karibu wanaume kumi wakiwa wamevalia sare, na mbele ya watoto wake walioandamana naye kutoka shule.

Naveed ni mtu wa tabaka maalum la wanafikra wa kisiasa wa Kiislamu ambao wana uwezo wa kipekee wa kutoboa joho la udanganyifu ambalo limetupwa kwenye mazingira ya kisiasa yanayooza. Hii ndio sababu Naveed aliweza kufikiria "**ramani halisi ya utendakazi**" ambayo nchi yake, Pakistan, ambayo anaipenda, inaweza kutambua ukuu wake. Ruwaza ambayo kwayo Pakistan inaweza kutumia vizuri faida zake za kijiografia, idadi ya watu, asili na za kiufundi na hivyo kuwa kituo cha mvuto katika Asia ya Kusini na Kati. Ruwaza ambayo kwayo Pakistan itaweza kuwa kituo cha nguvu kubwa katika Asia, na kufikia mwamko wa pili wa Umma wa Kiislamu, na kuzindua tena urithi wake ambao umeanza miaka 1,400.

Sababu ya ukosefu wa haki ambao Naveed alifanyiwa ni kukosoa kwake barabara maamuzi na matendo ya wanasiasa wakuu na maafisa, iwe serikalini au katika jeshi. Maamuzi na hatua ambazo, kwa upande mmoja, zilivuruga uwezo wa Pakistan, na kwa upande mwengine, zikivunja mshikamano wa karne nyingi kati ya jamii za Waislamu ambao walikuwa wameishi na kufanikiwa kwa muda mrefu katika sehemu hii ya Asia.

Moja ya msimamo wa ukosoaji wa Naveed ulikuwa ni juu ya vita jumla ambayo Pervez Musharraf aliendelea kupigana dhidi ya watu wa Magharibi mwa Pakistan. Jeshi la Pakistan lililazimika kupigana na kuua kaka na dada zake katika makabila ya eneo la FATA. Hii yote ilikuwa kwa ajili ya kupunguza shinikizo kwa jeshi la Amerika lililokuwa likiwakamata upande wa pili wa mpaka nchini Afghanistan. Vita vikali ambavyo vilidumu kwa miaka 17, ambavyo viliharibu miji, shule na nyumba, viliua makumi ya maelfu ya Waislamu, vilihamisha mamia ya maelfu yao, na kusababisha mpasuko mkubwa katika kitambaa cha jamii za Waislamu ndani ya Pakistan, ambacho bado kingali hakijatengenezwa.

Naveed aliwakosoa waziwazi majenerali mafisadi na maafisa vibaraka ambao wameruhusu kuenea hatari kwa ushawishi wa Amerika katika vituo nyeti zaidi vya taasisi za jeshi na serikali. Kila aina ya maafisa kutoka Shirika la Upelelezi la Amerika (FBI) na Shirika la Ujasusi la Amerika (CIA) walikuwa wamewekwa ndani ya idara ya "Makao Makuu ya Jeshi", "Kitengo cha Operesheni za Kijeshi" na "Ujasusi wa Ndani" za jeshi la Pakistan kwa ajili ya usimamizi na kudumisha udhibiti. Na hivi sasa, kwa msaada wa majenerali na wanasiasa mafisadi, Amerika inafanya maamuzi juu ya silaha za kinyuklia na za kawaida, na maamuzi ya vita na amani nchini Pakistan. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

*Endelea... UK 4*

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ إِن تُطِيعُواْ الَّذِينَ كَفَرُواْ يَرُدُّوكُمْ عَلَى أَعْقَابِكُمْ فَتَنقَلِبُواْ خَاسِرِينَ
“**Enyi mlio amini! Ikiwa mtawat'ii walio kufuru watakurudisheni nyuma, na hapo mtageuka kuwa wenye kukhasiri.**” [Surah Aali-Imran 3:149].

Tangu walipomteka nyara Naveed, serikali zote mtawalia nchini Pakistan zimekataa bila aibu kujulisha mahali alipo; Hawaja punguza hata kwa uchache mateso kwa wapendwa wake, kupitia kumleta hata kwa muda mchange ili akutane na familia yake. Kwa muongo mmoja, wameziba masikio yao kwa wito wa familia yake na ndugu zake katika Umma wa Kiislamu na kila mtu aliyehurumia mateso yake. Kinyume chake, wakala za ujasusi zilitoa vitisho kwa familia yake kwamba ikiwa Naveed hakuacha kazi yake ya kisiasa, atauawa na mwili wake kutupwa mahali pengine.

Tuko hapa leo, na baada ya kuingia katika mwaka wa kumi wa utekaji nyara wake, bado tunaendelea kutaka kuachiliwa huru kwake, na tunamtaka kila Muislamu, mkubwa au mdogo, wa karibu au wa mbali, kushiriki katika juhudi hii iliyobarikiwa. Utekaji nyara wa Naveed unawakilisha nukta ya mgongano kati ya mapenzi ya mwenye haki na mapenzi ya msaliti.

**Kwa Maafisa Wenye Ikhlasi na Watiifu katika Vyeo Vyote vya Jeshi la Pakistan:**

Someni ayah zinazoambatana na miito yenye kuyapamba mabega yenu. Kumbukeni mafundisho ya itikadi asili ya kivita ya jeshi lenu. Angalieni usaliti unaofanywa kwa kaka na dada zenu katika maeneo ya FATA, Jammu na Kashmir. Angalia kutokuchukua hatua kwa wanaodhulumiwa nchini Myanmar, Msikiti wa Al-Aqsa na Ukanda wa Gaza.

Tunakuulizeni... Tangu lini jeshi la Pakistan limekuwa jeshi la maneno matupu, sio jeshi la vitendo?! Je! Tangu lini walinzi wa Uislamu wamekuwa ni watazamaji tu wa matukio?! Je! Silaha mnazozibeba zinafaida gani ikiwa sio za kuzuia na kulipiza kisasi?! Kwa nini simba katika vikosi vya jeshi la Pakistan wanatanua nguvu zao juu ya ulimwengu badala ya juu ya uonevu wa sasa wa Amerika?!

Hakika Ndugu Naveed ni mmoja wa mashababu wanaojulikana kwa kujitolea kwao kwa hukmu za Uislamu na tabia njema, mwanafikra mwaminifu, na mwanasiasa mashuhuri ... Aliwasilisha ramani ya ukweli ya utendakazi ambayo ingeleta kheri na wokovu kwa Pakistan na nchi zote za Waislamu ulimwenguni ... Ramani ya Utendakazi ya Khilafah Rashida kwa njia ya Mtume Muhammad, (saw)... Lakini badala ya kumheshimu na kumthamini, watu mafisadi kati yenu walimteka nyara mahali kusikojulikana, La Hawla wala Quwatta illa Billah... Kwa hivyo, tunamtaka kila mmoja wenu mwenye ikhlasi kushinikiza mamlaka zinazohusika kwa ajili ya kuachiliwa huru haraka kwa Ndugu Naveed kurudi kwa familia yake, ili apande minbar na kusema ukweli pamoja na ndugu zake wengine katika Hizb ut Tahrir.

**Kwa Wanachama wa Ujumbe wa Kidiplomasia wa Pakistan:**

Nyinyi mnawakilisha sura, sifa, historia na hivi sasa watu wa Pakistan ulimwenguni. Kupotezwa kwa nguvu kwa Naveed kunachafua sifa ya haki katika nchi yenu. Kwa hivyo tunakulinganienì mufanye sehemu yenu katika kumaliza aibu hii ambayo serikali imejiletea.

**Kwa kila Muislamu anayetamani kuchomoza tena kwa siku za tukufu za Umma,**

**Kwa kila mwandishi wa habari ambaye amechukua jukumu lake kufichua uonevu na dhuluma,**

**Tunakulinganieni nyote:** njooni mjiunge na kampeni hii kuishinikiza serikali ya Pakistan na majenerali wa jeshi lake kumwachilia huru Naveed Butt na kumunganisha tena na familia yake.

Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَإِنِ اسْتَنصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ
“**Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia”** [Al-Anfal: 72].

**#FreeNaveedButt**

**Mh. Salah Eddine Adada**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI: Wakoloni wa Magharibi Kufadhili Elimu ili Kuendeleza Utumwa wa Kifikra

**Habari:**

Mnamo Ijumaa, 11 Juni 2021 Rais Uhuru Kenyatta alimpongeza Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson kwa kuahidi milioni £430 (takribani bilioni Ksh65) kwa kampeni ya Ushirikiano wa Kimataifa kwa ajili ya Elimu. Rais alisema kwamba Kenya inamshukuru Waziri Mkuu Boris Johnson na Uingereza kwa kuongoza mwito wa kufadhili elimu na kuwaunganisha viongozi wa dunia katika G7 na wengineo ili kuwekeza zaidi katika elimu kama njia ya kuongoza katika afueni na kujenga ubora wa kimataifa baada ya janga la Covid-19. [The Star, 11/06/2021]

**Maoni:**

Kwa hakika elimu ni moja katika zana msingi ambazo wakoloni wa Magharibi wanaendelea kuipatiliza katika kuyatia minyororo makoloni yao ya zamani. Ni kupitia elimu ndipo wakoloni wa Magharibi wanaendelea kutawala nchi za ulimwengu wa tatu kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Ili kuwadhibiti na kuwakoloni watu wa kiasili, wa Magharibi walianzisha utaratibu wa mchakato wa kuwaunganisha na moyo wake ukiwa ni elimu ya kisekula. Kuwaunganisha ilimaanisha wanaokoloniwa kulazimishwa kuendana na thaqafa na desturi ya wa Magharibi wakoloni.

Kilele cha uunganishaji kilikuwa ni udhibiti wa kithaqafa. Uthibiti wa kithaqafa umebakia ni mbinu ya kisiasa iliyo na ufanisi hadi sasa. Kwani inafanyakazi kwa kuridhia na aghalabu hutangulia uvamizi wa kinguvu. Hivyo basi, tawala za kikoloni za Magharibi zilipata nguvu kubwa sio kupitia udhibiti wa kimwili, bali kupitia udhibiti wa kifikra. Walisonga mbele na kutekeleza udhibiti huu hadaifu kupitia eneo la kujumuisha kifikra linalojulikana kama utaratibu wa shule.

Utaratibu wa shule unaendelea hadi sasa kutumika kuwaandaa watawala vibaraka wa kikoloni ambao wanapewa madaraka kupitia mlango wa nyuma kwa jina la 'uhuru bandia wa bendera!' kwa sharti kwamba watekeleze vipaumbele vya mabwana zao. Kwa hiyo, watawala vibaraka watiifu wa kikoloni wanaendelea kufuata nyayo za mabwana zao wa kikoloni wa Magharibi kwa kubuni sera na kanuni ambazo zinaongozwa kwa maslahi yao! Wale wanaoitwa wachache waliopendelewa na wafanyikazi wa serikali wanajivunia mabwana zao wa Magharibi kiasi kwamba wanakejeli thaqafa yao na raia wenzao!

Nia ovu kabisa ya elimu ya kikoloni ya kisekula ilifichuliwa na Thomas Babington Macaulay, pale aliposema, "Lazima hivi sasa tufanye kazi nzuri ya kubuni tabaka la watakao kuwa wakalimani baina yetu sisi na mamilioni ambao tunawatawala; tabaka la watu ambao kwa damu na rangi ni Wahindi, lakini Waingereza kihisia, kimtazamo, kimaadili na kifikra." Kwa maneno mengine, Macaulay alimaanisha kwamba miundo ya kujifunza ya asili ibadilishwe kwa ile ya wakoloni wa Magharibi! Dhati yake ikiwa ni kukuza vitambulisho vya kisekula vya kirasilimali!

Kwa kuzingatia ufupisho huo hapo juu, hakuna kheri inayotarajiwa kutokana na ahadi ya kifedha. Kwani Kenya imebakia kuwa koloni la Uingereza kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Pasina shaka huu mzunguko mpya wa msaada wa kielimu ni mbinu nyingine ya kikoloni kuwadhoofisha na kuwafanya watumwa raia wa koloni ili kubakia ndani ya sanduku la kisekula la kirasilimali! Hivyo basi, haishangazi kattu kwamba bwana Mkoloni na meneja wake kuwa wenyeji wa kongamano la siku mbili kuhusu ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya ufadhili wa elimu mnamo 25 – 26 Julai 2021. [The Star].

Iko njia moja pekee ya kupambana na hii kampeni ya elimu ya kisekula ya kikoloni ya wa Magharibi. Ni kwa kukumbatia na kufanyakazi ya mradi wa Khilafah. Mradi wa kimataifa unaongozwa na Hizb ut Tahrir. Chama cha kimataifa cha Kiislamu cha kisiasa ambacho kina jitahidi usiku na mchana ili kurudisha maisha ya Kiislamu kwa kurudiha tena Khilafah. Khilafah itatekeleza nidhamu ya elimu ambayo imechipuza kutoka kwa msingi wa itikadi (aqeedah) ya Kiislamu. Lengo la elimu ndani ya Khilafah litakuwa ni kujenga utambulisho (shaksiyyah) ya Kiislamu kifikra na kitabia. Hivyo basi, masomo yote katika mtaala yatachaguliwa kwa msingi huo. Kwa hiyo, itikadi ya kisekula, fikra za kidemokrasia, huria n.k. HAZITOKUBALIWA kama ilivyo leo ndani ya nidhamu zetu za elimu!

Elimu ndani ya Khilfah itakuwa ndio njia ya kuhifadhi thaqafa ya Ummah ndani ya mioyo ya watoto wake na kurasa za vitabu vyake, ima ni katika mtaala wa elimu uliopangiliwa. Mtaala wa elimu inamaanisha elimu iliyopangiliwa na nidhamu na kanuni ambazo Khilafah imejifunga nazo. Khilafah itakuwa na wajibu wa kuitekeleza mfano kuweka umri wa kuanza kusoma, masomo ya kufundishwa na njia ya elimu. Ilhali elimu ambayo haikuwekewa mpangilio itawachiwa Waislamu kufundisha majumbani, miskitini, vilabuni, kupitia vyombo vya habari na machapisho ya mara kwa mara. Hata hivyo, katika hali zote hizo Khilafah itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba fikra na maarifa (yanayo fundishwa) ima yanachipuza kutoka katika itikadi ya fikra ya Kiislamu au imejengwa juu yake. [Misingi ya Mtaala wa Elimu katika Dola ya Khilafah]

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



# Mfumo Huu Hautowalinda Waislamu wa Palestina

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**
**Fatima Musab**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

Mnamo Alkhamisi, 'Israel' na Palestina zilihakikisha kuwa zimekubaliana kwa kauli moja juu ya usitishaji wa mapigano, ambapo Raisi wa Amerika Joe Biden aliukaribisha kwa kuwa ni "fursa ya kweli ya kupiga hatua" kuelekea amani ya kudumu katika Mashariki ya Kati. (Chanzo) Siku iliyofuata, 'Israel' iliwashambulia Waislamu wa Palestina katika Al-Aqsa.

Msururu wa matukio yasitushangaze. Usitishaji wa mapigano hautosimamisha ukandamizaji unaowakumba Wapalestina - haukuwahi kabla, wala hautoweza sasa au siku za mbeleni. Mwaka 2014, makubaliano 9 ya kusimamisha vita yalikuja na kuondoka kabla mzozo kumalizika. (Chanzo) na msururu wa mashambulizi ya karibuni yanaonyesha kuwa makubaliano hayo yalikuwa ni masitisho ya muda tu.

**Msighilibiwe na miito kwa ajili ya usimamishaji - watawala wa sasa hutegemea rai jumla iwe upande wao.**

Watawala katika mfumo wa sasa hutegemea rai jumla iwe upande wao. Na shutuma kali za hivi karibuni dhidi ya 'Israel' zimekuwa sio za kawaida – kumekuwa na miito duniani kote, huku mitandao ya kijamii ikihanikiza taarifa zenye kueneza uelewa kuhusu hali katika Palestina. Pia wakivitaka vyombo vya habari vya kawaida kujitokeza kwa kuionyesha taswira potofu ya hali ilivyo au kwa vichwa vya habari ambavyo kwa makusudi vinatuondosha kutoka kiini cha tatizo – watu wa Palestina wanataabika, na 'Israel' inalindwa na mataifa duniani kote.

Kila siku zikipita, na dola kuanza kutoa matangazo ya kusitisha vita na kile kinachoitwa masuluhisho ya tatizo, ni muhimu kuwa tusiruhusu mazingatio yetu kufifia - usitishaji vita, hata ukiendelea kwa muda kiasi gani, hautobadilisha hali. Hautotatua tatizo, hautozuia Wapalestina kukandamizwa. Mabomu yanaweza kusita, lakini kuamiliwa kwao kuwa ni raia wa daraja la pili - na la tatu katika ardhi ambayo Mazayuni wanaikalia hakutobadilika.

**'Israel' inaikalia ardhi ya Palestina- na wanawachukia watu wake**

'Israel' imepewa ardhi ya Palestina mwaka 1948, kilele cha ahadi zilizotolewa na Uingereza (Pamoja na msaada wa dola nyengine) kwa Mazayuni katika Azimio la Balfour. Kwa kipindi kirefu, 'Israel' imekuwa ikitumia jeshi kueneza udhibiti wao, kukalia ardhi ya Palestina na kuwafanyia uadui mkubwa watu wa Palestina.

Viongozi wa 'Israel' hata hawalifichi hili.

*Wapalestina ni kama Wanyama, sio binaadamu (MK Ben Dahan, Naibu Waziri wa Zamani wa Ulinzi)*

*"Wapigeni, sio mara moja, bali mara nyingi, wapigeni ili wapate maumivu sana, hadi isiweze kuvumilika"* Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu

Uongozi unazidi kusisitiza kuwa 'Israel' ni dola ya Kiyahudi, na makaazi ya Mayahudi kwenye ardhi ya Palestina ni "thamani kuu ya dola hiyo". Na uzoefu wa Wapalestina (katika) "uhamishwaji kwa nguvu,

***Endelea... UK 7***

upokonywaji wa ardhi, hadhi duni kisheria na vifungo ni hali halisi inayowakumba Wapalestina wote, ima wa 'ndani' ya 'Israel' au katika maeneo yaliyokaliwa kimabavu." (Chanzo) Walowezi wa 'Israel' katika Ukingo wa Magharibi uliokaliwa wanaruhusiwa kubeba silaha, na mara nyingi wanawashambulia Wapalestina pamoja na majumba yao na mashamba. (Chanzo)

**Upigaji mabomu unaweza kusita lakini hali ya maisha ya Wapalestina ni ya kuogofya**

Mnamo 2012, Umoja wa Mataifa ulieleza kuwa Gaza inaweza isikalike, isipokuwa hali itengemae. Tokea muda huo, hali imekuwa mbaya- na sio nzuri. (Chanzo) Ukingo wa Gaza "umegeuzwa kuwa ni suala la ufadhili kwa maafa makubwa na utegemeaji misaada na uwezo wa uzalishaji wa Gaza umevurugwa na operesheni kubwa tatu na kudhoofishwa angani, baharini na kizuizi cha ardhini." (Chanzo)

Ripoti ya 2018 imesema kuwa kuna "rasilimali chache kwa maendeleo na uchocheaji wa uchumi wa uzalishaji." Mapato halisi ya sasa katika Gaza ni asilimia 30 chini zaidi ya ilivyokuwa mwanzoni mwa karne hii. Kwa wastani, familia zinapata masaa 2 tu ya umeme kwa siku. (Chanzo)

Ripoti ya karibuni ya BBC imefichua kuwa ufungaji wa 'Israel' umeathiri "nyendo za kuingia na kutoka kwenye Ukingo na uwezo wa kufanya biashara." Watu wengi katika Gaza wanasumbuliwa na uhaba wa maji na zaidi ya watu milioni moja katika Gaza wanawekwa kuwa ni "waathirika wa wastani wasio na uhakika wa chakula" licha ya kuwa wengi hupokea aina fulani ya msaada wa chakula.

'Israel' inazuia upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo na uvuvi, ambapo hupunguza kiasi cha chakula ambacho watu wa Gaza huweza kuzalisha wenyewe. Hawaruhusiwi hata kulima katika "eneo la amani lililotangazwa na Israel". 'Israeli' pia imeweka ukomo katika uvuvi, inayoathiri fursa za chakula na ajira ndani ya Gaza. Hata hivyo, mnamo wiki chache zilizopita, 'Israel' ilizuia uvuaji wa Samaki kutoka Ukingo wa Gaza moja kwa moja.

Huduma za afya ziliharibiwa au kuvurugwa, kutokana na mashambulizi ya 'Israel' ndani ya miaka kadhaa. Ndani ya Gaza, kwa upande mwengine ni "gereza huru la anga", pindi wagonjwa wakihitaji matibabu katika Ukanda wa Magharibi au hospitali za Jerusalem ya Mashariki lazima kwanza watake maombi yanayohakikiwa na Mamlaka ya Palestina na kisha yapate ruhusa ya serikali ya 'Israel' – katika mwaka 2019, kiwango cha maombi ya wagonjwa waliotaka kuondoka Ukanda wa Gaza yaliokubaliwa yalikuwa ni 65% (Chanzo)

**Hatuwezi kusahau shida zao- wala tusiruhusu nafsi zetu kuchanganyikiwa**

Waislamu wa Palestina wanahangaika, wamekuwa katika mihangaiko kwa miongo kadhaa na wataendelea kuhangaika hadi hali itatuliwe.

Lakini vipi tunaweza kuuamini mfumo ambao umezalisha tatizo, kuleta suluhisho. Uwepo wa Israel ni kwa sababu Mfumo wa Kirasilimali wa Kiliberali umewapa ardhi, umewahalalishia mamlaka yao juu yake na kwa majivuno unailinda kutokana na kila aina ya matokeo halisi.

Dola ndani ya mfumo huu zitaendelea kufanya hivyo, hata kama 'zitalaani' namna wanavyo watendea watu wa Palestina wanaume, wanawake na watoto.

Na vipi tunaweza kutarajia tahafifu yoyote?

Wakati mfumo unawashajiisha watawala 'kusawazisha' mahusiano na 'Israel' hadi kufikia watawala hawa wanaoitwa wa Waislamu kuweka maslahi ya kibiashara na kisiasa mbele ya maisha ya wanaume, wanawake na watoto?

Wakati mfumo ukiruhusu kwa dhihaka orodha ndefu ya ukatili- nje na ndani ya Palestina? Orodha ya ukatili ambayo haipo tu katika historia bali inahisiwa na Waislamu duniani kote hivi leo, na katika dakika hii.

Kama tupo makini kuhusiana na kuwasaidia ndugu zetu wa kike na wa kiume na kutimiza Faradhi ya kuzihifadhi ardhi za Waislamu na damu zao, tunahitajia kubadilisha mfumo. Kwa sababu ni kwa kuisimamisha tena dola ya Khilafah pekee ndipo Waislamu wa Palestina watakuwa na hifadhi na haki wanayostahili kuipata.

**إِنَّمَا الْإِمَامُ جُنَّةٌ يُقَاتَلُ مِنْ وَرَائِهِ وَيُتَّقَى بِهِ فَإِنْ أَمَرَ بِتَقْوَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ وَعَدَلَ كَانَ لَهُ بِذَلِكَ أَجْرٌ وَإِنْ يَأْمُرْ بِغَيْرِهِ كَانَ عَلَيْهِ مِنْهُ**

**"Hakika Imamu ni ngao, hupiganwa nyuma yake na hujikinga kwake, basi akiamrisha kwa taqwa ya Mwenyezi Mungu Aliyetukuka na akafanya uadilifu atakuwa na ujira kwa hilo na kama ataamrisha kwa chengine kisicho hicho atakuwa dhidi yake."** (Muslim)

**#الأقصى_يستصرخ_الجيوش**

**#Aqsa_calls_armies** **#AqsaCallsArmies**

**#OrdularAksaya**

**#AqsaYawaitaMajeshi**

 Email: info@uqab.or.ke

# Masuali 3 kwa Majeshi ya Waislamu Kutoka kwa Vijana wa Kiislamu wa Magharibi

Sisi, vijana wa Kiislamu wa Magharibi, tumefanya kila kitu ndani ya uwezo wetu kuzuia uvamizi. Utawaona maelfu ya vijana wa Kiislamu wakilaani, kuandamana, wakitumia majukwaa yao ya mitandao ya kijamii, hata kufikia kufukuzwa mashuleni kwa msimamo wao wa kutoomba radhi.

Sisi, vijana wa Kiislamu wa Magharibi, tunataka kuweka wazi kuwa tunapinga usitishaji wowote wa mapigano na umbile hili la Kiyahudi lililo na madhara. Hakuna usitishaji wa mapigano na umbile hili ovu ambalo halikuuletea Ummah huu isipokuwa balaa kwa zaidi ya miaka 70. Usitishaji utafanyika tu baada ya umbile hili dhalimu kufutwa na kuwekwa bendera ya Uislamu. Sio kupitia kwa Waislamu waliozingirwa wa Gaza, wanaojihami kwa maroketi wala kwa Waislamu waliokaliwa kimabavu katika Ukingo wa Magharibi, wanaojihami kwa mawe, kuweza kuzikomboa ardhi takatifu. Wajibu unawaangukia wale wenye uwezo wa kupigana na majeshi, kama majeshi ya Waislamu wa Uturuki, Misri, Sudan, Tunisia, Pakistan, Bangaldesh na Indonesia.

**Enyi Majeshi ya Waislamu!** Ndugu zenu na dada zenu wa Magharibi wana maswali 3 kwenu:

**1. Je, mna nyoyo za mawe?**

Nyoyo zenu hazipati maumivu kwa ajili ya ndugu yenu aliyewaangalia mabinti zake wawili machoni, akiwadanganya kwa kuwaahidi watakuwa sawa, (haya yote) kutokana na makombora ya kuangamiza ya Mazayuni?

Nyoyo zenu hazichuriziki damu kwa ajili ya dada yenu ambaye matumaini yake na ndoto zake za baadaye zikizikwa ndani ya vifusi pamoja na mtoto wake aliye tumboni?

Nyoyo zenu hazivunjiki kwa ajili ya wavulana na mabinti zetu wakikimbia kujiliwaza kwenye mikono ya mama zao ikiangamizwa kiungo baada ya kiungo?

Au mmekaa ndani ya kambi zenu na nyoyo za mawe?

Enyi Majeshi ya Waislamu! Hamna 'Izzah (utukufu) kwa Mola wetu, Kiongozi wetu, RasulAllah (saw)?

Haukuwa Msikiti wa Al-Aqsa ambao Yeye (saw) aliongoza Mitume (ahs) katika Swalah?

Vipi mnavumilia kiburi na majivuno yao wakati Mitume (ahs) wakisimama kwa Khushuu' (unyenyekevu)?

Vipi mnawaruhusu kuitikisa ardhi wakati nyoyo za Mitume zikitingishika kutokana na kisomo chake (saw)?

Vipi mnaruhusu viatu vyao vichafu kukanyaga mahala ambapo uso Wake Mtukufu (saw) ulisujudu?! Chukizo la aibu mno linatokea kwenye utazamaji wenu!

Au mmezama kiasi cha kukosa ambacho kimewafanya kuwa kama maadui zetu na maadui zenu ambao nyoyo zao zimekuwa ngumu kuliko mawe?

**ثُمَّ قَسَتْ قُلُوبُكُم مِّن بَعْدِ ذَلِكَ فَهِيَ كَالْحِجَارَةِ أَوْ أَشَدُّ قَسْوَةً وَإِنَّ مِنَ الْحِجَارَةِ لَمَا يَتَفَجَّرُ مِنْهُ الأَنْهَارُ وَإِنَّ مِنْهَا لَمَا يَشَّقَّقُ فَيَخْرُجُ مِنْهُ الْمَاء وَإِنَّ مِنْهَا لَمَا يَهْبِطُ مِنْ خَشْيَةِ اللّهِ وَمَا اللّهُ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ**

**Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo, hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi, kwani kuna mawe yanayochimbuka mito, na kuna mengine yanayopasuka yakatoka maji ndani yake, na kuna mengine huanguka kwa sababu ya khofu ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na mnayoyafanya." [Al Baqarah:74]**

**2. Je, mmevunja ahadi yenu na Mwenyezi Mungu (swt)?**

Enyi Majeshi ya Waislamu! Mlipojiunga na Uaskari wa Ummah huu mtukufu, mliungana na urithi wa miaka 1400 iliopita wa Mujahidiin kutokea wakati wa Masahaba (rah) na utaratibu huo utaendelea hadi siku ya hukumu. Mmeweka ahadi na Mwenyezi Mungu (swt) kuitumikia Dini Yake, na sio kuhudumia mipaka ya kitaifa iliochorwa na makafiri wakoloni. Mmeweka ahadi kumtii Mwenyezi Mungu (swt) na sio kuwatii watawala wenu walio watiifu wa fikra za kijinga jinga. Mumeweka ahadi, enyi Majeshi ya Kiislamu, kuulinda Ummah!

**وَإِنِ اسْتَنصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ**

**"Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia…"** [Al Anfal: 72]

Hamuhisi aibu kuwa Ummah umeweka matumaini kwenu?

Hamuhisi aibu kuwa wanawake wanapigana badala yenu?

Hamuhisi aibu kuwa Mola wenu amekuulizeni nyinyi zaidi ya mara moja:

"Nini kinakusibuni?"

**وَمَا لَكُمْ لاَ تُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللّهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاء وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ هَذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ أَهْلُهَا وَاجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ وَلِيًّا وَاجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ نَصِيرًا**



Email: info@uqab.or.ke

**“Na mna nini msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanaoonewa, wanaume, wanawake na watotot, ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu, na tujaalie tuwe na mlinzi anaetoka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anye toka kwako.”** [An-Nisa:75]

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمُ انفِرُواْ فِي سَبِيلِ اللّهِ اثَّاقَلْتُمْ إِلَى الأَرْضِ أَرَضِيتُم بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الآخِرَةِ فَمَا مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الآخِرَةِ إِلاَّ قَلِيلٌ**

**“Enyi Mlioamini! Mna nini mnapo ambiwa: Nendeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu mnajitia uzito katika ardhi? Je mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache.”** [At-Tawbah:38]

Mnang'ang'ania ardhi yenu (iliochorwa) ya kikoloni, hata hamvuki mipaka hiyo linapokuja suala la kuuliwa kwa wingi ndugu zenu wa kike na kiume? Je, huu ni urithi mnaotaka kuwaachia watoto wenu na watoto wao? Je, hamna uoni kwa ajili ya Uislamu?

Enyi majeshi ya Waislamu! Kama hamtazivunja pingu hizi ambazo zimeweka udhalilifu na fedheha juu ya Ummah huu basi mtafikwa na adhabu kali na mtabadilishwa badala yenu kwa watu wengine walio bora.

**إِلاَّ تَنفِرُواْ يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا وَيَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلاَ تَضُرُّوهُ شَيْئًا وَاللّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ**

**“Kama hamwendi atakuadhibuni adhabu chungu, na atawaleta watu wengine, wala nyinyi hamtamdhuru chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”** [TMQ At-Tawbah: 39]

Enyi majeshi ya Waislamu! Msiivuje ahadi yenu kwa Mwenyezi Mungu (swt)! Msiwe kama maadui zetu na maadui zenu!

**وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ وَرَفَعْنَا فَوْقَكُمُ الطُّورَ خُذُواْ مَا آتَيْنَاكُم بِقُوَّةٍ وَاسْمَعُواْ قَالُواْ سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا وَأُشْرِبُواْ فِي قُلُوبِهِمُ الْعِجْلَ بِكُفْرِهِمْ قُلْ بِئْسَمَا يَأْمُرُكُمْ بِهِ إِيمَانُكُمْ إِن كُنتُمْ مُّؤْمِنِينَ**

**“Na tulipochukua ahadi yenu na tukauinua mlima juu yenu (tukakwambieni). Kamateni kwa nguvu haya tuliyokupeni na sikieni, wakasema tumesikia na tumekataa! Na wakanyweshwa nyoyoni mwao (imani ya) ndama kwa kufuru yao. Sema ni uovu mno iliyokuamrisheni imani yenu ikiwa ni wenye kuamini.”** [TMQ Al-Baqarah:93]

3. Hivyo nyinyi mnatilia shaka ahadi ya Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume Wake (saw)?

Hayo mawe yanayorushwa, yakipigana badala yenu dhidi ya maadui wenu, karibuni yatawadhihirikia. ‘Abdulla bin Umar (ra) amepokea: Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akisema, “Mayahudi watapigana na nyinyi, na mtapata ushindi dhidi yao ambapo jiwe litasema, ‘Ewe Muislamu! Kuna Yahudi nyuma yangu; muuwe!” (Sahih al Bukhari). Umbile la Kiyahudi karibuni litaangamizwa na mahala pake patakuwa Mji Mkuu wa Khilafah. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema: Suala hili (Khilafah) litakuwa baada yangu katika Madinah, kisha Al-Sham, kisha Jazira, kisha Iraq, kisha katika Madinah, kisha katika Bayt ul-Maqdis. Itakapokuwa katika Baytul Maqdis, basi hapo ni nyumbani kwake, na hakuna watu watakaoweza kuiondosha, hivyo itarejeshwa kwao moja kwa moja.” (Ibn Asakir, Tarikh Dimashiq 368)

Enyi majeshi ya Waislamu! Msiwe kama maadui zetu na maadui zenu wanaoshuku ahadi ya Mwenyezi Mungu (swt).

**يَا قَوْمِ ادْخُلُوا الأَرْضَ المُقَدَّسَةَ الَّتِي كَتَبَ اللّهُ لَكُمْ وَلاَ تَرْتَدُّوا عَلَى أَدْبَارِكُمْ فَتَنقَلِبُوا خَاسِرِينَ * قَالُوا يَا مُوسَى إِنَّ فِيهَا قَوْمًا جَبَّارِينَ وَإِنَّا لَن نَّدْخُلَهَا حَتَّىَ يَخْرُجُواْ مِنْهَا فَإِن يَخْرُجُواْ مِنْهَا فَإِنَّا دَاخِلُونَ * قَالَ رَجُلاَنِ مِنَ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَنْعَمَ اللّهُ عَلَيْهِمَا ادْخُلُواْ عَلَيْهِمُ الْبَابَ فَإِذَا دَخَلْتُمُوهُ فَإِنَّكُمْ غَالِبُونَ وَعَلَى اللّهِ فَتَوَكَّلُواْ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ * قَالُواْ يَا مُوسَى إِنَّا لَن نَّدْخُلَهَا أَبَدًا مَّا دَامُواْ فِيهَا فَاذْهَبْ أَنتَ وَرَبُّكَ فَقَاتِلا إِنَّا هَاهُنَا قَاعِدُونَ**

**"Enyi watu wangu ingieni katika nchi takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amekuandikieni. Wala msirudi nyuma, msije mkawa wenye kukhasirika. Wakasema: ewe Musa! Huko wako watu majabari . nasi hatutaingia huko mpaka wao watoke humo. Wakitoka humo hapo tutaingia. Watu wawili miongoni mwa wachamngu ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha, walisema: Waingilieni kwa mlangoni. Mtakapo waingilia basi kwa yakini nyinyi mtashinda. Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini. Wakasema: Ewe Musa! Sisi hatutaingia humo kamwe maadamu wao wamo humo. Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa."**
[TMQ Al-Maidah: 21-24]

Enyi majeshi ya Waislamu, tunakuulizeni masuala haya 3 mepesi, je, kuna yeyote ataejibu? Hatuhitaji kuyasikia majibu yenu, enyi majeshi ya Waislamu! Tunahitaji kuyaona majibu yenu.

**#Aqsa_calls_armies** **#AqsaCallsArmies**

**#OrdularAksaya** **#الأقصى_يستصرخ_الجيوش**


**#AqsaYawaitaMajeshi**

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Syed Fahad**

**JIBU LA SWALI**

# Je, Yajuzu kwa Mwanamke Kafiri Kutawalishwa Ukadhi wa Shariah?



**Swali:**

Assalam Aleykum wa Rahmatullah wa Barakatuh. Sheikh mpendwa, natumai Mwenyezi Mungu atakamilisha amri yake mikononi mwenu na atukirimu kwa Dola ya Khilafah karibuni, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu juu ya hilo… na hapa nina hamu ya kujua hali katika kusimama Dola yetu je, tutampa mwanamke kafiri mamlaka ya kuwa Kadhi wa Shariah?

Niko na swali, imetajwa katika kitabu cha Nidhamu ya Kijamii ukurasa 91 kwamba yajuzu kwa mwanamke kuwa na mamlaka ya kuhukumu kwa lafdhi ya hadith ambayo ni jumla,

لنْ يُفْلِحَ قومٌ ولّوا أمرَهُمُ امرأةً

"**Hawatafaulu watu watakaompa mwanamke mamlaka ya mambo yao**", na kikasema hii ni dalili ya kujuzu kwake kuwa kadhi… imenipitikia mawazoni mwangu; kwamba mwanamke kafiri au katika watu wa kitabu yajuzu kwake kuwa na mamlaka ya kuhukumu… wala sijawahi kupata andiko kuwa mwanamke asiyekuwa Muislamu alitawalishwa ukadhi katika Uislamu kwa wale waliotangulia… ni nini maana ya hilo? Na je, yajuzu kwa mwanamke kafiri kuwa na mamlaka ya kuwa kadhi wa Shariah? Na hapa nakusudia (sheria ya) hali za kibinafsi; ndoa, talaka… na tumefafanua maana ya ukadhi kuwa ni ujulishaji hukmu kwa njia ya ulazima… na je, kutoitakidi hukmu ni njia ya ulazima? Na kuhitimisha nataraji utakuwa na subira kwa swali hili na utanifikishia jibu la kutosheleza. Na daima muwe katika kheri elfu moja na namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa uwezo awahifadhi kutokana na kila ovu.

**Husam Dawoud / Palestina**

**Jibu:**

Waaleykum salaam wa rahmatullah wa barakatuh,

Inaonesha kana kwamba unaashiria andiko lifuatalo katika kitabu, Nidhamu ya Kijamii mlango "Kazi za Mwanamke":

(… Isipokuwa kwamba haijuzu kwa mwanamke kuchukua wadhifa wa utawala, hasi hawezi kuwa raisi wa dola, wala Mu'aawin (msaidizi) wake, wala Wali (gavana), wala 'Aamil (meya wa mji), wala kazi yoyote inayo chukuliwa kuwa ya utawala, kutokana na yale yaliyo simuliwa kutoka kwa Abu Bakrah aliyesema: Pindi habari zilipomfikia Mtume (saw) kwamba watu wa Fursi wamemtawaza ufalme binti ya Kisra alisema:

لنْ يُفْلِحَ قومٌ ولّوا أمرَهُمُ امرأةً

"**Hawatafaulu watu watakaompa mwanamke mamlaka ya mambo yao**", [Imepokewa na Bukhari]. Na hii iko wazi katika katazo la kumpa mwanamke utawala kwa kuwashutumu wale wanaotawalisha mambo yao kwa wanawake. Na mtu mwenye mamlaka (Wali al-amr), ni mtawala asema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنْكُمْ

***Endelea... UK 11***

 **Email: info@uqab.or.ke**

“**Enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi**”. [An- Nisaa`: 59]

Hivyo basi mamlaka ya utawala hayajuzu kwa wanawake, ama usiokuwa utawala yajuzu kumpa mamlaka hayo mwanamke. Kwa hayo, yajuzu kwa mwanamke kuteuliwa katika nyadhifa za utumishi wa umma katika dola, kwa sababu hizi sio katika utawala bali zinaingia katika mlango wa ajira, hivyo basi mfanyikazi huyo ni mwajiriwa wa kibinafsi wa serikali, na yeye ni kama mwajiriwa wa mtu au shirika lolote, na inajuzu kwake kuwa kadhi kwa sababu kadhi si katika watawala bali yeye huondoa utesi baina ya watu, na huwajuza hukmu ya kisheria wanaozozana kwa njia ya ulazima. Hivyo basi ufafanuzi wa ukadhi ni ujulishaji hukmu kwa njia ya ulazima. Hivyo basi kadhi ni mfanyikazi na sio mtawala, yeye ni mwajiriwa wa dola kama waajiriwa wengine. Na imesimuliwa kutoka kwa Umar bin Al-Khattab kwamba alimpa mamlaka al-Shifa - mwanamke katika jamaa zake - ya soko yaani kadhi wa masoko (Qadhi al-Hisbah ambaye anahukumu juu ya ukiukaji wote. Na kwamba suala la mwanamke kujuzu kuwa kadhi linahusiana na andiko la hadith hiyo na kutekelezeka juu ya uhalisia wa wadhifa wa kadhi. Ikiwa hadith ya katazo la kumpa mwanamke utawala inatabikika juu ya ukadhi basi kumpa mamlaka hayo ya ukadhi itakuwa haijuzu, na ikiwa haitabikiki juu yake basi hadith hii haitasihi kuwa ni dalili ya kumkataza kuwa kadhi. Na tunapoiangalia hadith hii tunapata kuwa Mtume (saw) aliwashutumu watu waliotawalisha mambo yao kwa mwanamke, kama jibu kwa yale yaliyomfikia kwamba watu wa Fursi wamemtawaza ufalme mwanamke juu yao, hii ni taaliki juu ya habari, na mahali pa jibu la swali. Hivyo hii ni maalum kwa maudhui ya uraisi wa dola, na maana yake ni utawala. Hii ni kwa upande mmoja, na kwa upande mwengine katazo limenasibishwa na utawala jumla, kwa sababu huo ndio utawala wa mambo (ya watu). Hii ndio maana ya hadith hii na lile inalofahamisha. Ama maudhui ya ukadhi ni kazi ambayo yatofautiana na kazi ya Khalifah na Wali (gavana). Kazi ya Khalifah na Wali ni utekelezaji hukmu moja kwa moja kwa upande wake, sawa iwe kadhia imeletwa kwake, au kuletwa kwa kadhi, au iwe kadhia haikuletwa kwake na yeyote, lakini akaona kuwa kuna ukiukaji wa sheria, basi atahukumu ukiukaji huo pasi na kuwepo mlalamishi na atatekeleza hukmu juu yake kwani yeye ni mtekelezaji. Ama kadhi yeye hana uwezo wa kuhukumu isipokuwa inapopatikana kesi, kupitia mlalamishi kumpelekea kesi, na kukawa na watesi wawili. Basi atahukumu kesi hiyo. Na hakuna atakalofanya endapo hakutakuwepo na mlalamishi. Na kwa mtazamo wake wa kadhia, atajulisha hukmu ya kisheria katika kadhia hiyo kwa njia ya ulazima, wala kamwe hana mamlaka ya utekelezaji, isipokuwa ikiwa ameteuliwa kama mtawala na kadhi wakati huo huo, basi hapo atatekeleza kwa sifa yake kama mtawala na atahukumu kwa sifa yake kama kadhi. Na kwa hilo, uhalisia wa ukadhi sio uhalisia wa utawala, hivyo hadith hii haitabikiki juu ya kadhi…" Mwisho.

Swali lako ndugu yangu haliko wazi na ndani yake mna mambo yaliochanganyika, je unauliza kuhusu hukmu ya kumpa mamlaka ya ukadhi wa Kisheria mwanamke kafiri katika upande wa kuwahukumu baina ya Waislamu? Au unakusudia hukmu ya kumpa mwanamke mamlaka ya ukadhi kuhukumu baina ya makafiri katika watu wa dini yake katika mambo ya ndoa na talaka ambayo Shariah imejuzisha kuhukumu kwao katika mambo hayo kwa mujibu wa dini zao?

1- Ama kuhusu hali ya kwanza nayo ni kuhukumu baina ya Waislamu, hiyo haijuzu kwa mwanamke kafiri kuwa kadhi baina ya Waislamu katika swala lolote kama ambavyo haijuzu kwa mwanamume kafiri kuwa kadhi baina ya Waislamu katika suala lolote **na hilo ni kwa sababu masharti ya kadhi wa kisheria ni awe ni Muislamu sawa awe ni mwanamume au mwanamke,** kwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلاً

“**…Wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini**. [An-Nisa: 141]. Hivyo ndani yake kuna katazo la kukatikiwa kwa sababu semi hii ina herufi "Lan (kamwe)" ambayo inaashiria mwiko, ni maelezo kwa maana ya ombi, na maadamu Mwenyezi Mungu ameharamisha kafiri kuwa na mamlaka juu ya Waumini basi ameharamisha kumjaalia kafiri kuwa kadhi anayehukumu baina yao, kwani katika kuhukumu ni kuwa na mamlaka juu ya Waislamu. Na tumetaja sharti la Uislamu upande wa kadhi katika zaidi ya sehemu moja katika vitabu vyetu, kwa mfano:

**- Katika kitabu cha *Taasisi za Dola ya Khilafah* mlango "masharti ya makadhi":**

(Ni sharti kwa yeyote anayechukua wadhifa wa ukadhi awe: Muislamu, mtu huru, aliye baleghe, mwenye akili timamu, mwadilifu, msomi wa fiqhi, mjuzi wa kuvua hukmu juu ya uhalisia.) Mwisho.

**- Katika kitabu cha *Utangulizi wa Katiba*, Juzuu ya kwanza:**

**(Kifungu cha 78: ni sharti kwa yeyote anaye chukua wadhifa wa ukadhi kuwa: Muislamu, mtu huru, aliye baleghe, mwenye akili timamu, mwadilifu, msomi wa fiqhi, mjuzi wa kuvua hukmu juu ya uhalisia. Ni sharti kwa yeyote anaye chukua wadhifa wa kadhi mwenye kutatua dhulma za watawala kwa raia (Kadhi al-Madhaalim) awe na masharti ziada ya haya awe mwanamume na awe Mujtahid.**

Dalili zake ni dalili iliyo tangulia ya kadhi mkuu, isipokuwa si sharti kwa kadhi anaye tatua tetesi wala kadhi wa masoko awe mwanamume, bali yajuzu kuwa mwanamke;

***Endelea... UK 12***

kwa sababu yeye si mtawala bali ni kadhi, yaani yeye ni mjulishaji tu wa hukmu ya kisheria na sio mtekelezaji wake; na kwa hilo hadith:

«لَنْ يُفْلِحَ قَوْمٌ وَلَّوْا أَمْرَهُمُ امْرَأَةً»

"**Hawatafaulu watu watakaompa mwanamke mamlaka ya mambo yao**", iliyo pokewa na Bukhari haitabikiki juu yake, kwani hiyo ni katika mamlaka ya utawala, na sababu ya hadith hii ni tukio la watu wa Fursi kumtawaza ufalme mwanamke juu yao. Kutoka kwa Abu Bakrah amesema: Pindi ilipomfikia Mtume (saw) kwamba watu wa Fursi wamemtawalisha ufalme binti wa Kisra alisema:

«لَنْ يُفْلِحَ قَوْمٌ وَلَّوْا أَمْرَهُمُ امْرَأَةً»

"**Hawatafaulu watu watakaompa mwanamke mamlaka ya mambo yao**" imepokewa na Bukhari. Hivyo basi sababu ya kauli ya hadith hii ni maudhui maalum yaliyo tajwa waziwazi katika andiko la hadith nayo ni utawala yaani mamlaka, na ukadhi sio katika utawala, hivyo basi hadith hii inakuwa ni maalum kwa utawala pekee wala haijumuishi ukadhi…) Mwisho.

2- Ama kuhusu hali ya pili shariah imeijuzisha dola kuwapa wadhifa wa ukadhi raia wasiokuwa Waislamu (*Ahlu al-dhimma)* katika mambo yanayowahusu wao kwa wao kulingana na dini zao katika ndoa na talaka na yanayohusiana nayo… makadhi wa Kiislamu hawatahukumu baina yao kwa shariah ya Kiislamu wala kwa sheria zao, bali hukumu baina yao itatolewa na makadhi miongoni mwao yaani wasiokuwa Waislamu, lakini watu hawa watatengewa mahakama maalum, bali watakuwa na vyumba vya mahakama ndani ya majengo ya mahakama za dola na zitakuwa chini ya idara ya mahakama za dola, wala hawataachwa kujiteulia makadhi wenyewe lakini utaratibu huo utakuwa ni wa dola. Hivyo basi, dola ndio itakayo teuwa miongoni mwao makadhi watakaohukumu baina yao katika mambo ya ndoa na talaka na yanayo husiana nayo, kwa mujibu wa dini na sheria zao, kama shariah ilivyo idhinisha.

Ikiwa sheria zao zinaruhusu kadhi mwanamke kuhukumu baina yao katika mambo ya ndoa na talaka basi inawezekana basi kuteuliwa wanawake makafiri kuwa miongoni mwa makadhi ambao dola itawateua kuhukumu baina ya watu wa dhimmi, yaani itawezekana kwa mwanamke kafiri katika hali hii kuwa kadhi atakaye hukumu baina ya watu wa dini yake kulingana na sheria zao…

Nataraji kwamba hili litakuwa ndio jibu la maswali yako, na Mwenyezi Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Zaidi na Mwingi wa Hekima.

**Ndugu yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**